TEKNOLOJIA

NA ROMANA MALLYA

# TEHAMA inavyotupa mbali bajeti ya karatasi, shughuli zote kielektroniki

TANGU kuanzishwa kwa Mamlaka Serikali Mtandao (e-GA) mafanikio mbalimbali yamepatikana, kama ujenzi na matumizi ya rasilimali shirikishi za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwa taasisi za umma.

Umejengwa Mfumo wa Baruapepe Serikalini (GMS) unaotumiwa na taasisi 770 na Mfumo wa Huduma za Serikali kupitia simu za Mkononi (mGov) unaotumiwa na taasisi 429.

Ni kwa mujibu wa Mkurugenzi Mkuu wa e-GA, Benedict Ndomba, anayeutaja pia Mfumo wa Ofisi Mtandao (GeOS) unaotumiwa na taasisi 347 pamoja na Mtandao wa Mawasiliano Serikalini (GovNet) ambao umeunganisha ofisi 457 za umma.

Mafanikio hayo ni miongoni mwa mengi anayoyaainisha katika kikao kazi cha tano cha Serikali Mtandao, kilichofanyika jijini Arusha hivi karibuni.

Kikifunguliwa na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan na kufungwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, ujenzi wa mifumo na mafanikio ni masuala yanayojiri.

Mkurugenzi Mkuu wa e-GA, anataja mengine ya kujivunia kuwa ni ujenzi wa mifumo tumizi ya kisekta na kitaasisi kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali ikiwamo Mfumo wa Kusimamia Rasilimali Watu Serikalini (New HCMIS).

Anasema mfumo huo ulijengwa kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ambao unatumiwa na taasisi 466 kati taasisi 530.

"Pamoja na mifumo ya fedha iliyojengwa kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na taasisi zake, ambayo ni: Mfumo wa Malipo Serikalini (GePG), wa Kusimamia Hesabu za Serikali (MUSE), mwingine ni wa Kusimamia Mali za Serikali (GAMIS), upo wa kuwezesha miamala ya malipo (TIPS)," anasema.

Ndomba anawaambia washiriki kuwa mamlaka imeziwezesha taasisi za umma kutoa huduma mtandao kupitia mifumo ya TEHAMA, kama tovuti mbalimbali kama ya Tovuti Kuu ya Serikali, ya Ajira na Mfumo wa Bunge Mtandao (e-Parliament).

Anaeleza kuwa mifumo hiyo sio tu imerahisisha utendaji kazi pia imeboresha utoaji wa huduma kwa umma na kulinda mazingira kwa kupunguza matumizi ya karatasi, ambayo pia yamepunguza gharama za kuendesha serikali.



Mkurugenzi Mkuu wa e-GA, Benedict Ndomba. **PICHA: ROMANA MALLYA.**

Ndomba anawaambia kuwa ujenzi na uendeshaji wa mifumo na miundombinu hiyo, hufanywa kwa kutumia wataalamu wazawa na imeokoa fedha nyingi za zilizotumika kununua mifumo kutoka kwa wakandarasi wa nje kwa gharama kubwa.

Anabainisha kuwa, mamlaka imewajengea uwezo maofisa TEHAMA serikalini, kwa kuwapa mafunzo ya mara kwa mara kuhusu utekelezaji wa Serikali Mtandao kutokana na mabadiliko ya teknolojia yanayotokea duniani.

"Hatua hii imewasaidia wataalamu wetu kuendelea kuwa na ujuzi zaidi, pamoja na kuongeza hali ya kujiamini katika tasnia hii ya TEHAMA."

Ndomba anasema kuanzishwa kwa mamlaka hiyo kumeiwezesha serikali kuwa na udhibiti wa moja kwa moja wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA inayotumika serikalini, sambamba na kulinda usalama wa taarifa za serikali.

Anaongeza kuwa katika kukabiliana na matishio ya usalama wa mtandao, mamlaka hutoa msaada wa kiufundi na ushauri kuhusu usalama wa TEHAMA.

Pia, anasema hutoa msaada wa viashiria vya matishio ya kiusalama mtandaoni kwa taasisi za umma, pamoja na kukabiliana na mashambulio ya kimtandao pindi yanapotokea.

"Yote haya hufanyika kwa kutumia wataalamu wa ndani ambao wanahusika moja kwa moja katika kujenga, kusimamia na kuendesha jitihada za Serikali Mtandao katika taasisi za umma.

"Wataalamu hawa wamewezesha kutatua baadhi ya matatizo yetu kupitia mifumo ya TEHAMA waliyoisanifu, kuijenga na kuiendesha wenyewe, ambayo inatumika katika taasisi za umma kama nilivyoeleza hapo awali," anaongeza.

Ili kuhakikisha mifumo na miradi ya TEHAMA serikalini inaleta tija iliyokusudiwa, mamlaka huandaa viwango na miongozo ya Serikali Mtandao, ambayo taasisi za umma zinatakiwa kuifuata wakati wote wa uandaaji na uendeshaji wa miradi hiyo, anawaambia washiriki.

Na katika jitihada za kuendana na mabadiliko ya teknolojia yanayotokea duniani, mwaka 2019, mamlaka ilianzisha Kituo cha Utafiti, Ubunifu na Uendelezaji wa Serikali Mtandao (eGovernment Research, Innovation and Development Centre - eGOVRIDC), kwa mujibu wa maelezo yake.

Anasema kituo hicho, hufanya tafiti na bunifu mbalimbali za mifumo ya TEHAMA, inayolenga kutatua changamoto zilizopo, ili kuboresha utendaji kazi serikalini na utoaji wa huduma kwa umma.

Mkurugenzi Mkuu wa e-GA, anaeleza mamlaka inakitumia kufuatilia matumizi ya teknolojia mpya zinazoibuka na kuangalia namna zinavyoweza kupata matokeo chanya.

"Ili kufikia malengo haya, mamlaka imesaini makubaliano ya ushirikiano (MoU) na taasisi za elimu ya juu pamoja na zile za utafiti 14 zikiwamo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, UDOM, pamoja na Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar (eGAZ) katika matumizi na usimamizi wa TEHAMA," anasema.

Anataja baadhi ya mifumo iliyojengwa kupitia kituo hicho ni, Mfumo wa Uendeshaji wa Vikao kwa njia ya Mtandao (e-Mikutano), wa mawasiliano kati ya wananchi na serikali (e-mrejesho).

Anasema e-mrejesho unatambuliwa na Umoja wa Mataifa kama mfumo bora unaoiunganisha serikali na wananchi kidijitali na kuiwezesha serikali kufanya maamuzi kwa wakati.

Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, katika hotuba yake, anataka vipaumbele vya e-GA visimamiwe ipasavyo na kusisitiza utekelezaji wa agizo ambalo mara kadhaa Rais Samia analitoa la mifumo ya kusomana na kubadilishana taarifa.

"Jambo hili ni muhimu ili kurahisisha utendaji kazi katika taasisi za umma na utoaji huduma kwa wananchi.

"Nimeridhishwa na utendaji kazi wa e-GA katika kutekeleza agizo hili kwa kusanifu na kujenga mfumo mkuu wa ubadilishanaji taarifa Serikalini wa GovESB.

"Hakikisheni taasisi nyingi za umma zinaunganishwa na kubadilishana taarifa kupitia mfumo huu," anasema.

Dk. Mpango ametaka pia, suala la uzingatiaji wa sheria, kanuni, viwango na miongozo ya serikali mtandao katika uanzishaji na uendelezaji wa miradi yote ya TEHAMA serikalini.

Aidha, Waziri Simbachawene anasema serikali imetoa kipaumbele kwenye matumizi ya TEHAMA, hususani katika masuala ya utafiti ya ubunifu, ili kuimarisha usalama wa mtandao wa mawasiliano na kuongeza watumiaji wa intaneti.

Wizara kupitia e-GA, imejipanga kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma mtandao kwa umma kidijitali, sambamba na kuboresha upatikanaji wa huduma za serikali kupitia simu za mkononi nchi nzima, ili kuwawezesha Watanzania kupata huduma kwa wakati na kwa gharama kupitia mifumo ya TEHAMA, anaeleza.

"Tunajivunia kuona idadi ya watumiaji wa simu za mkononi pamoja na intaneti inaongezeka mwaka hadi mwaka.

"Ongezeko hili linatupa chachu ya kuboresha upatikanaji wa huduma za serikali kupitia simu za mkononi na linadhihirisha ongezeko la matumizi ya TEHAMA hapa nchini," anaongeza.

Waziri Simbachawene anazitaka taasisi za umma kuchukua hatua za haraka ili kuhakikisha zinatumia fursa ya ongezeko hili kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi kidijitali kupitia simu za mkononi.

Kadhalika, anaielekeza e-GA kuendelea kufanya utafiti ili kuleta bunifu za mifumo ya TEHAMA, ambayo sio tu itaboresha utendaji kazi bali pia, itasaidia kuondoa kero za upatikanaji wa huduma mbalimbali za serikali kwa wananchi.

Makamu Mwenyekiti Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao, Dk. Jasmine Tiisekwa, anasema mamlaka iko tayari kupokea maelekezo ili kuijenga serikali.